

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI

04 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI – TAREHE 04 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

179. MHESHIMIWA HASSAN SELEMANI MTENGA (MTWARA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara za lami katika Kata za Ufukoni, Magomeni na Shangani Manispaa ya Mtwara Mikindani.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

180. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-
Vitendo vya rushwa vimekithiri katika Mchezo wa Soka hapa nchini:-

Je, ni kwa kiasi gani Serikali inakabiliana na kudhibiti hali hiyo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**181. MHESHIMIWA HUSNA JUMA
SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na
Watoto:-

Je, Serikali inatumia njia gani kuwawezesha
Wanawake Wajasiriamali kupata mafunzo
ya ujasiriamali, uandaaji wa maandiko ya
miradi na kuwaunganisha na Taasisi za
Kifedha ili wapate mikopo.

WIZARA YA KILIMO:

**182. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT
KAIZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwekeza
kwenye kilimo cha umwagiliaji katika Mikoa
ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Tabora,
Singida, Dodoma na Morogoro ili kuongeza
mazao ya kilimo yatakayosafirishwa kupitia
SGR.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

183. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Sera na Mitaala shirikishi ili kuwa na msingi wa aina moja kuanzia Elimu ya Maandalizi, Elimu Msingi na Sekondari kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ili kuongeza ufaulu zaidi kwa upande wa Zanzibar.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

184. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itakuja na mpango maalum wa kurasimisha makazi ya Wananchi wa Mabwepande, Nakasangwe, Chasimba, Chatembo, Chachui, Ndumbwi, na Jogoo ili kumaliza migogoro ya ardhi na kuiongezea mapato Serikali.

WIZARA YA NISHATI:

185. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji 127 vilivyobaki vya Mkoa wa Songwe.

186. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Mwamalole, Mbushi, Mwamanongu, Imalaseko, Mwamanimba, Mwabuzo na Kimali ili Wananchi waweze kufaidika na huduma hiyo na kuchochea maendeleo katika Kata hizo.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

187. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya mpakani kutoka Mtawanya kwenda

Nanyumbu kupitia Mpilipili – Mapili – Chikoropola – Lichele – Lupaso hadi Lipumburu.

188. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara inayounganisha Jimbo la Ukonga na Mbagala kwa mkupuo badala ya kujenga kilomita 1 kila mwaka ili kuondoa kero ya usafiri kwa Wakazi wa Majimbo hayo.

WIZARA YA MAJI:

189. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya ujenzi wa Mradi mkubwa wa Maji wa *Handeni Trunk Main (HTM)*.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA
04 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**

